

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1575,
Simu: (026) 2700157
Nukushi: (026) 2703014
Barua pepe: rbciringa@pccb.go.tz
Mtandao : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

IRINGA 10 JULAI, 2020

**TAKUKURU IRINGA YAMKABIDHI MASHINE YA KUCHANGANYIA ZEGE
YENYE THAMANI YA SH. 6,321,000 MWANANCHI ALIYEDHULUMIWA KWA
NJIA ZA RUSHWA**

Ndugu wanahabari,

Katika kutekeleza operesheni zake za ufuatiliaji na urejeshwaji wa fedha zinazofanyiwa ubadhirifu na ukiukwaji wa taratibu katika Taasisi mbalimbali kwa njia za rushwa ikiwepo na Taasisi zinazojishughulisha na mikopo umiza, TAKUKURU Mkoa wa Iringa mnamo tarehe 29/06/2020 imefanikiwa kurejesha mashine ya kuchanganyia zege (concrete mixer) yenye thamani ya Shilingi **6,321,000/-** (Milioni sita, mia tatu ishirini na moja elfu) kwa mwananchi aitwae **Mtalemwa John Kaiza** ambaye ni mmiliki wa Kampuni ya Lekashingo Construction Company Ltd.

Ndugu wanahabari,

Bw. Mtalemwa John Kaiza mnamo tarehe 30/10/2018 alikopa Shilingi 2,000,000/- kutoka kwa Bw. Abel Muyinga ambaye ni mkopeshaji wa mikopo umiza, na mara baada ya kukopa fedha hizo alitakiwa amkabidhi mashine yake ya kuchanganya zege (concrete mixer) na ilipofika tarehe 12/02/2019 alikuwa amerejesha kiasi cha Shilingi **2,250,000/-**. Baada ya marejesho hayo kufanyika mkopeshaji huyo wa mikopo umiza alimueleza kuwa deni lake limefikia kiasi cha Shilingi **7,000,000/-** Hivyo deni lake lililobaki ambalo alitakiwa kulipa ni Shilingi 5,000,000/-. Aidha, baada ya hapo aliendelea kushikilia mashine hiyo

huku akiwa anaikodisha kwa kipiondi chote na fedha iliyopatikana aliendelea kuitumia kwa manufaa yake binafsi. Ndipo TAKUKURU ilipoingilia kati na kuweza kuirejesha mashine hiyo kwa mmiliki Bw. Mtalemwa John Kaiza.

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatoa wito kwa Taasisi binafsi zikiwamo za kutoa mikopo kwa wananchi, kutojihusisha na vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka pamoja na uvunjifu wa Sheria na kanuni zinazoendesha Taasisi hizo.

Pia inawaasa wananchi wote wanaofanyiwa vitendo kama hivi vinavyokiuka Sheria na taratibu watoe taarifa TAKUKURU mara moja ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika .

Imetolewa na:

SGN

Mweli E. Kilimali

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa